

جمعية الدعوة والإرشاد وتنمية الجاليات بالزلفي

مشروع تعلم الإسلام - أحكام الصلاة - سواحيلي

Samo la 10

الدرس العاشر

RAKAA MBILI ZA ALFAJIRI.

Miongoni wa sunnah zinazo ambatana na swala za faradhi alizokuwa mtume (saw) akidumu nazo akiwa safari au akiwa hayuko safari ni rakaa mbili kabla ya alfajiri.

عن عائشة رضي الله عنها : ((أن النبي - صلى الله عليه وسلم - لم يكن على شيء من المواقف، أشد معااهدة منه، على ركعتين قبل الصبح)) [متفق عليه: 1163، 724] (Hadithi aliyoipokea mama Aisha (R.A) anasema: Hakika ya Mtume (saw) hakuwa na kitu chochote katika sunnah alichofungamana nacho, zaidi ya rakaa mbili za sunnah kabla ya swala ya subhi) (Ameipokea Imamu Muslim : 1163, 724).

ولقوله - صلى الله عليه وسلم - : ((لهم أحبب إلَيَّ من الدنيا جميًعا)) [روايه مسلم: 725]

(Na kauli yake Mtume katika kuzzungumzia rakaa mbili hizi: (Ya kwamba ninazipenda zaidi kuliko dunia yote) (Ameipokea Imamu Muslim : 725).

Ni sunnah unaziswaliraka mbili hizi kusoma rakaa ya kwanza Surat Fat-ha na Surat Kafiruna (قل هو الله أحد) na rakaa ya pili Surat Fat-ha (قل يأيها الكافرون) mara nyingine anaweza kusoma rakaa ya kwanza (قُولُوا آمَنَّا بِاللَّهِ وَمَا أُنْزِلَ إِلَيْنَا الْآتِيَة) na katika rakaa ya pili ataisoma ayah hii: (فُلُّ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْا إِلَى كَلْمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ...)

Kama ilivyo sunishwa kuziswali kwa kuzihafifisha, kwa aliyofanya Mtume (saw)nna inafaa kwa yule aliyeipita na hizi rakaa mbili za kabla ya alfajir, atazikidhi baada ya swala , na ni bora azikidhi kabla ya kuchomoza kwa jua na liwe ziko kiasi cha urefu wa mkuki mpaka kufikia kabla ya wakati wa makatazo muda wa kuwa jua kumili.

SWALA YA DHUHA.

Nayo ni swala ya wenye kurejea kwa Allah (sw) (wenye kutubia), ni sunnah iliyositisizwa zimepokelewa hadithi nyingi za kutilia mkazo juu ya swala hii.

Hadithi ya Abu Dharri (R.A) mtume (saw) anasema :

عن أبي ذر رضي الله عنه ، عن النبي - صلى الله عليه وسلم . أنه قال: «يُصْبِحُ عَلَى كُلِّ سَلَامٍ (أي: مفصل) مِنْ أَحَدِكُمْ صَدْقَةٌ ، فَكُلْ تَسْبِيحَةً صَدْقَةٌ ، وَكُلْ تَهْمِيلَةً صَدْقَةٌ ، وَكُلْ تَكْبِيرَةً صَدْقَةٌ ، وَأَمْرٌ بِالْمَعْرُوفِ صَدْقَةٌ ، وَنَهْيٌ عَنِ الْمُنْكَرِ صَدْقَةٌ ، وَبِجَزِئِهِ مِنْ ذَلِكَ رَكْعَاتٌ يَرْكَعُهَا مِنَ الْضَّحْيَةِ » [روايه مسلم: 720]

(Mtume (saw) anasema: Kinapambaukiwa kila kiungo cha mmoja wenu kuwa ni swadaka, kila tasbihi ni sadaka, na kila tahmiid ni swadaka, na kila tahlil ni swadaka, na kila takbir ni swadaka, na kuamrisha mema ni swadaka, na kukataza maovu ni swadaka, na imalipwa kutokana na hayo rakaa mbili anazoziswali za Dhuha) (Ameipokea Imamu Muslim: 820).

وعن أبي هريرة - رضي الله عنه . قال: ((أوصاني خليلي بثلاث ، لا أدعهن حتى أموت: صوم ثلاثة أيام من كل شهر ، وصلاة الضحي ، ونوم على وتر)) [متفق عليه: 1178، 721].

(Hadithi ya Abu Huraira (R.A) anasema : (Ameniusia kipenzi changu mambo matatu nisiachane nayo mpaka nife, ameniusia kufunga siku tatu za kila mwezi, na swala ya Dhuha na kulala nikiwa nimeswali swala ya witri) (Ameipokea Bukhar na Muslim: 1178 , 721).

Wakati mzuri wa kuiswali swala ya Dhuha ni pale jua litakapo nyanyuka kiasi cha mkuki, na jua likawa ninachoma na wakati wake unatoka pindi jua litakapo mili upande wa magharibi, na uchache wa rakaa zake ni rakaa mbili na wala aina kiwango maalum.